

KILIMO CHETU MARIDHAWA

Ni dhahiri kwamba kilimo ni uti wa mgongo katika maendeleo endelevu hapa nchini Tanzania, hii ni kutokana na uchumi na shughuli za wananchi walio wengi kujihusisha na sekta ya kilimo, hivyo serikali ya Tanzania kupitia wizara ya kilimo inahakikisha kuwepo kwa miundombinu na sera bora za kilimo .

Aidha, kulingana na sera ya Serikali ya awamu ya tano ya Maendeleo ya Viwanda sekta ya kilimo imepewa kipaumbele na inatakiwa kuboreshwa ili kuendana na kasi ya maendeleo endelevu katika sekta ya viwanda, hivyo wananchi wanaaswa kushirikiana na serikali kuhakikisha suala hili linafanikiwa, hasa nguvu kazi.

Hata hivyo, idara ya kilimo katika Manispaa ya Musoma inaundwa na sehemu tatu ambazo ni Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika ambapo mazao yanayolimwa ni mbogamboga, Matunda, Mihogo, Viazi vitamu , Mpunga , Mahindi, na Mazao jamii ya mikunde.

Wakazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma hawajitoshelezi kwa chakula kinachozalishwa katika eneo la Manispaa kutokana na eneo linalolimwa kuwa dogo hivyo kusababisha uhitaji wa kuingiza chakula kutoka mikoa na wilaya jirani kwa kununua, kisafirisha na kuuzwa kwenye masoko yaliyopo Manispaa.

Katika Manispaa hii kilimo hufanywa na wakulima wadogo, maeneo wanayolimwa ni yenye ukubwa kati ya ekari 1/8 ya ekari hadi ekari 5 .

Pia katika mpango wa kuendeleza kilimo wilaya iliviwezesha vikundi viwili kununua vitalu nyumba viwili ambayo vinatumia kulima mazao ya mbogamboga. Aidha wadau wa maendeleo 3 wamenunua vitalu nyumba vitatu ambavyo vina tumika kuzalisha mazao ya mbogamboga.

Hata hivyo, vitalu nyumba hivyo, kitalu nyumba kimoja kilichopo eneo la maonyesho la kilimo mseto kinatumika kuwafundishia wakulima matumizi teknolojia ya kitalu nyumba, uzalishaji wazao la nyanya katika baadhi ya vitalu nyumba unakabiliwa na ugonjwa wa mnyauko Fuzari.

Kwa kipindi cha Julai 2017 hadi Mei 2018 jumla ya vitalu nyumba vitatu vimeendelea kuzalisha mazao ya mbogamboga aina ya nyanya, matango, chainizi na sukumawiki. Hivyo basi Halmashauri inaendelea kuwahamasisha wakulima kulima kwa kutumia vitalu nyumba.

Wananchi wa Manispaa ya Musoma wanajihusisha na shughuli za kilimo cha umwagiliaji ambacho kinafanyika kandokando ya Ziwa Victoria na katika maeneo ya makazi kwa kutumia njia mbalimbali za umwangiliaji, mazao yanayozalishwa kwa njia ya umwangiliaji ni yale ya mbogamboga.

Kufikia Mei 2018 jumla ya wakulima 124 wamefundishwa kutumia njia mbalimbali za umwangiliaji kulingana na maeneo wanayolima, njia zilizo fundishwa ni umwangiliaji kwa njia ya matone katika vitalu nyumba na mashamba ya wazi, umwangiliaji kwa njia ya mafuriko kwa zao la vitunguu na mpunga.

Pia Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imekwisha vipatia mafunzo vikundi 4 vinavyojishughulisha na uotesaji wa miche ya

aina mbalimbali za matunda.Vikundi hivyo ni 'Panda zote' na 'Rejeshwa misitu' vilivyopo katika kata ya Kitaji na kata ya Nyakato.

Hali kadhalika Manispaa ya Musoma inao wafanyabiashara wanao nunua na kusafirisha mazao ya kilimo aina mbalimbali kutoka wilaya na mikoa jirani kwa kusudi la kuyasindika ili kuyaongezea thamani na kuyafungasha.

Halmashauri inakumbana na changamoto mbalimbali zikiwemo Bajeti finyu inayotengwa haitoshelezi mahitaji kwajili ya kutekeleza shughuli za idara ya kilimo.

Aidha, Kuendelea kuwepo kwa magonjwa ya muhogo ya Batobato na Michirizi kahawia kunachangia kupungua kwa uzalishaji wa zao la muhongo,Mabadiliko ya tabia ya nchi yanayo sababisha kutokutabilika kwa misimu ya mvua pia kuathili kiwango chamvua inayonyesha,kujitokeza kwa funza wanao shambulia zao la mahindi.

Katika kutekeleza mradi huo idara inaomba kuongezewa fedha itakayotengwa kwa matumizi ya kawaida,wakulima waelimishwe kuhusu magonjwa ya mihogo na kuhimizwa kutumia mbegu kinzani dhidi ya ugonjwa wa Batobato kali na Michilizi kahawia,wakulima wanashauliwa kulima mazao yanayostahimili ukame , mazao aina ya mbogambogana mazao yanayo komaa kwa muda mfupi kwa njia ya umwagiliaji.

Hivyo, Manispaa ya Musoma inashilikiana bega kwa bega na idara ya kilimo kuhakikisha kinachangia maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla.

Hivyo basi katika kufikia malengo endelevu kupitia sekta ya kilimo ili kuinua uchumi wa viwanda, sekta binafsi na jamii kwa ujumla vinapaswa kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano katika kufikia uchumi wa viwanda.